



## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

### USAJILI WA WAHUDUMU WA MABASI KWA MUJIBU WA SHERIA

*Dar es Salaam, 14 Agosti, 2024*

Kwa mujibu wa Kifungu cha 5(1)(e) cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini Sura ya 413, Mamlaka ina jukumu la kusajili wahudumu na kuthibitisha madereva wa vyombo vya moto vinavyotoa huduma za usafiri kibiashara.

Kanuni ya 17 ya Kanuni za Uthibitishaji Madereva na Usajili Wahudumu wa Magari ya Biashara za Mamlaka ya Udhibiti usafiri Ardhini (LATRA) za mwaka 2020, zinamtaka mtu yeyote anayekusudia kufanya kazi ya uhudumu katika gari linalotoa huduma za usafiri kibiashara kusajiliwa na LATRA.

#### FAIDA ZA WAHUDUMU KUSAJILIWA

- i. Kurasmisha fani na ajira ya wahudumu wa vyombo vya moto kibiashara
- ii. Kuongeza uwajibikaji katika kutoa huduma kwa mujibu wa Sheria
- iii. Kujenga ari ya umoja na mshkamano wa wahudumu hao katika masuala ya haki na wajibu wao

Katika kutekeleza matakwa ya Sheria na Kanuni tajwa hapo juu, Mamlaka inawatangazia watoa huduma za usafiri wa magari ya abiria ya masafa marefu kuwahimiza wahudumu waliowaajiri kupata mafunzo kutoka Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) au Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE). **Baada ya mafunzo, wahudumu hao watatakiwa kuwasilisha maombi ya kusajiliwa LATRA kwa ajili ya kupatiwa Kadi ya Usajili ya Mhudumu kwa mabasi ya abiria. Mamlaka inaendelea kusajili, kutoa elimu na kuratibu mafunzo ya wahudumu kwa kushirikiana na vyo husika.**

**Tarehe ya mwisho kwa wasafirishaji kutumia wahudumu ambao hawajasajiliwa na LATRA ni 31 Disemba, 2024.**

Mamlaka inawakumbusha wahudumu wote ambao wamepata mafunzo, kutuma maombi ya kusajiliwa kupitia <https://rrims.latra.go.tz/login> kwa kutumia Namba ya Kitambulisho cha Taifa (NIDA) au kufika ofisi yoyote ya LATRA. Maombi yaambatishwe na Cheti cha mafunzo na picha mbili za paspoti zenye kivuli cheupe.

Aidha, Mamlaka inapenda kuwajulisha wadau wa usafirishaji kuwa, ili kuhamasiha utoaji wa huduma bora na salama za usafiri wa mabasi ya mikoani nan chi jirani, imeandaa tuzo za mtoa huduma bora na sasa inaendelea kupokea maoni hadi tarehe 19 Agosti, 2024. Washindi watatangazwa katika kilele cha Wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani 26 Agosti hadi Mosi Septemba, 2024.

Salum Pazy

**MKUU WA KITENGO CHA UHUSIANO NA MAWASILIANO**

**Mafunzo hayo yatafanyika kwa ratiba ifuatayo:-**

<b>Na.</b>	<b>CHUO</b>	<b>KANDA</b>	<b>MKOA</b>	<b>TAREHE</b>
1	NIT	Kanda ya Ziwa	Mwanza	12-16 Agosti, 2024
		Kanda ya Kaskazini	Arusha	02-07 Septemba, 2024
		Dar es salaam	Dar es salaam	07-12 Oktoba, 2024
		Kanda ya Mashariki	Morogoro	04-09 Novemba, 2024
2	CBE	Kanda ya Kati	Dodoma	Julai/Agosti,2024
		Kanda ya Ziwa	Mwanza	Agosti/Septemba,2024
		Dar es salaam	Dar es salaam	Septemba/Oktoba,2024
		Kanda ya nyanda za juu Kusini	Mbeya	Oktoba/Novemba,2024